# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) JUU YA UWASILISHAJI WA RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** kwa unyenyekevu mkubwa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima wa kuweza kudiriki kufika na kushiriki katika kikao hiki cha Mkutano wa Nane tukiwa wazima na wenye afya njema, kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu kwa niaba ya wananchi waliotuchagua kuja hapa Barazani kuwawakilisha kwa kupaza sauti zao kwa maslahi yao na Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuzungumzia machache na ya muhimu, yanayohusu uwasilishaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar kwa mwaka 2020/2021, kama ambavyo Kanuni ya 43(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 inavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kuweza kuwasilisha hapa Barazani Ripoti hizi za Ukaguzi za mwaka 2020/2021 ambazo pamoja na mambo mengine ndizo nyenzo kuu tunazozitumia katika utekelezaji wa kazi za Kamati zinazosimamia masuala ya fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee natoa pongezi na shukurani za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kwa umoja, ushirikiano na ari kubwa waliyonayo hususan wakati tulipoanza kuipitia kazi hii hadi kuwasilisha kwangu hotuba hii fupi ya uwasilishaji wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2020/2021. Ni ukweli usiopingika kuwa mashirikiano na moyo wao wa kujituma ndio chachu inayoifanya Kamati hii kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wao, naomba kuwatambua kwa majina Wajumbe na makatibu hao wa Kamati yetu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Juma Ali Khatib - Mwenyekiti;
2. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - M/Mwenyekiti;
3. Mhe. Mihayo Juma Nh'unga - Mjumbe;
4. Mhe. Maryam Thani Juma - Mjumbe;
5. Mhe. Sulubu Kidongo Amour - Mjumbe;
6. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman - Mjumbe;
7. Ndg. Maryam Haji Ali - Katibu; na
8. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu.

**Mheshimiwa Spika,** kadhalika, nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa dhati viongozi na watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya za kufuatilia mapato na matumizi ya fedha za umma zinazotumika kwa shughuli mbali mbali za uendeshaji wa Serikali, Ofisi hii imefanya kazi kubwa na nzito ya kufanya ukaguzi katika Mawizara, na Taasisi mbali mbali za Serikali, na kuandaa Ripoti hizi kama ambavyo kifungu cha 112 cha Katiba yetu kinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** madhumini makubwa ya kuwepo kwa Taasisi hizi za kiukaguzi ni kuleta twasira nzuri kwa wananchi katika kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumika kama ilivyokusudiwa. Aidha katika kuhakikisha kwa kiasi gani taasisi za ukaguzi zinaleta tija katika maisha ya wananchi wetu hutegemea uwezo wa Taasisi hizo kuongeza uwajibikaji, uaminifu na uadilifu kwa Serikali na Tasisi husika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulifahamisha Baraza lako Tukufu kuwa Ukaguzi hupima usahihi na usawa wa taratibu za utunzaji wa Hesabu za Taasisi za Serikali pamoja na taarifa za fedha zilizotolewa na Taasisi hizo. Aidha, Ukaguzi hupima kama fedha zilitumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kwa kufuata Sheria, na taratibu zilizopo. Vile vile, Ukaguzi huchambua uhalali wa gharama, ufanisi wa mbinu zilizotumika, na ubora pamoja na ufanisi wa mipango ya Serikali kwa ujumla katika kufikia malengo iliyojiwekea. Zaidi ya hayo, kwa kutoa Ripoti hizi za Ukaguzi kwa Vyombo vinavyowakilisha wananchi kama hiki kupitia Serikali, Taasisi za Ukaguzi zinatoa fursa muhimu ya uwazi katika usimamizi na uendeshaji wa masuala ya fedha za Serikali kwa umma.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na maendeleo mbalimbali ulimwenguni yakiwemo ya Sayansi na Teknolojia, Uchunguzi wa Hesabu katika sekta za umma umekuwa ukibadilika siku hadi siku katika eneo la Ukaguzi hususan wa mapato na matumizi ya fedha kama ulivyowekewa misingi yake katika taratibu na Sheria za fedha na manunuzi.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mabadiliko hayo, Kamati yetu bado inaendelea kusisitiza kwamba upatikanaji wa mafunzo ya mara kwa mara kwa Kamati hizi ni jambo la msingi yakiwemo mafunzo ya mbinu na aina mbalimbali za Ukaguzi kwa Kamati hizi zinazosimamia masuala ya Kifedha ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hizi.

**Mheshimiwa Spika**, tukijikumbusha yaliyopita ambapo kulikuwa kunafanyika maovu

mengi ya kiutendaji lakini hakukuwa na ukaguzi uliyokuwa ukiibuwa kiuwazi kasoro zilizotokana na tuhuma za ubadhirifu na uhujumu wa mali za umma hadi kufikia Kamati yako ya kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Serikali kueleza wazi ndani ya Baraza hili kwamba 'yupo wapi CAG' wakati masuala hayo yalipokuwa yakitokea. Majibu ya suali hilo sasa yameanza kuonekana kwamba kumbe CAG yupo na anatekeleza wajibu wake wa kikatiba na kisheria hadi kufikia lengo la kutuwasilishia Ripoti hizi nzuri na muhimu katika mustakabali wa maendeleo ya nchi na wananchi wetu kiujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Kamati ya PAC imebaini kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetekeleza kwa vitendo na kwa ufanisi wa hali ya juu kilio cha siku nyingi cha kufanya ukaguzi na kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Miradi ishirini (20) ya Maendeleo ya Serikali inayotekelezwa na Serikali pamoja na Wahisani wa Maendeleo. Uwasilishaji huu, utaipa nafasi Kamati yako ya PAC kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Serikali kwa kufuatilia na kuchunguza kasoro zilizoibuliwa ili kupata taswira halisi kuhusiana na utekelezaji wake, changamoto zinazoikabili miradi hiyo, thamani halisi ya fedha za umma zilizotumika pamoja na usahihi na uhalisia wa kasoro ambazo zimeelezwa katika Ripoti hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kiujumla kutokana na uwasilishaji wa Ripoti ya CAG kwa mwaka 2020/2021, Kamati ya PAC inahusika zaidi na ufuatiliaji wa Ripoti tatu kati ya Ripoti Sita zilizowasilishwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinazohusiana na Ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu, Ripoti kuhusiana na Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo pamoja na Ripoti kuhusiana na Ukaguzi Maalum kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.

**Mheshimiwa Spika,** taswira ya jumla inaonesha wazi kwamba kuna kasoro nyingi zilizoibuliwa ambazo ziliainishwa katika Ripoti ya mwaka 2019/2020 pamoja na Ripoti za Ukaguzi Maalum uliofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kujirudia kwa kasoro hizo kunaonesha wazi kwamba bado kuna changamoto katika usimamizi na udhibiti wa fedha za umma unaofanywa na Maafisa Masuul ambao ndio wahusika wakuu. Aidha, kunatoa taswira kwamba baadhi ya watendaji wa Serikali na taasisi zake wamekosa uaminifu na uadilifu katika utekelezaji wa dhamana walizokabidhiwa kwa kwenda kinyume na matakwa ya sheria za usimamizi wa fedha za umma na sheria za Ununuzi badala yake wameendekeza maslahi binafsi yanayopelekea kutumia vibaya rasilimali za umma kwa kuneemesha wachache.

**Mheshimiwa Spika**, nikinukuu maneno ya hotuba ya Muasisi wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Aman Karume aliyesema 'kwa makosa madogo madogo tunatakiwa tusameheane lakini kwa makosa makubwa tupeane adhabu nzito'. Hivyo kuna kila sababu kwa wote walioshiriki kutumia rasilimali za umma kwa maslahi binafsi kuchukuliwa hatua za kisheria ili umma uone kwamba Serikali yao ipo makini na haiungi mkono vitendo vinavyorudisha nyumba maendeleo ya wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa kasoro zilizojitokeza katika ukaguzi uliopita lakini pia zimejitokeza tena katika ukaguzi wa mwaka huu wa 2020/2021 ni pamoja na kasoro katika ukaguzi wa malipo ya Pencheni Jamii. Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi milioni 2,720,000 ilibainika kuwa ni bakaa ya fedha ya malipo ya Pencheni Jamii ambazo hazikuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2019/2020 wakati katika ripoti iliyowasilishwa mwaka huu jumla ya shilingi milioni 51,804,687 zimegundulika hazikuwasilishwa Serikalini. Kwa upande wa kasoro katika ukaguzi wa Mashamba ya Mikarafuu, jumla ya shilingi milioni 830,476,000 zimebainika kuwa ni malimbikizo ya madeni ambayo hayakulipwa na Wakulima wa Mashamba hayo kwa mwaka jana wakati jumla ya shilingi milioni 66,125,000 zimebainika katika mwaka huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kasoro nyengine zilizobainika kujirudia ni pamoja na kutokukatwa kwa kodi ya zuio, kukosekana kwa hati za malipo kwa ukaguzi, malipo yasiyokuwa na mikataba au vielelezo pamoja na utunzaji mbaya wa kumbukumbu. Kamati ya PAC haikufurahishwa na kujirudia tena kasoro hizo kwani tulitegemea watendaji watakuwa wamejifunza na kujirekebisha kwa makosa waliyoyafanya awali lakini bado kasoro za aina hiyo hiyo zimejitokea tena.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imegundua kuwa ukaguzi uliowasilishwa umekuja na matokeo mengine mapya ambayo hayakuripotiwa katika ukaguzi uliopita wa mwaka 2019/2020. Kuainishwa kwa kasoro hizo mpya ambazo zinaathiri utendaji wa Wizara na Taasisi zake na kupoteza fedha nyingi kwa mambo yasiyo ya msingi kama ilivyopangwa katika bajeti ya mapato na matumizi ya Serikali, kutatoa funzo litakalowafanya Maafisa Masuul kupata moyo wa kujituma zaidi katika kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha za umma wanazokabidhiwa na kudhibiti mianya inayosababisha kasoro hizo kujitokeza.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa kasoro hizo ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwa ununuzi wa mafuta ambayo watendaji wakuu huyatumia kwa shughuli zao binafsi wakati posho la mafuta huingizwa katika maslahi yao, wapiganaji wa Idara Maalum kutopatiwa stahiki zao wakati wanapopatiwa uhamisho. Ukiukwaji wa sera na matoleo rasmi yanayotolewa na Serikali pamoja na kasoro za ukaguzi katika matumizi ya fedha za Uviko - 19.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa msingi huo, Kamati ya PAC ambayo ni moja ya Kamati za Kusimamia Masuala ya Fedha, itazifanyia kazi ipasavyo Ripoti hizi za Ukaguzi na hatimae kuwasilisha Ripoti yake kwa kina hapa Barazani katika muda muafaka, kama Katiba na Sheria za nchi hii, pamoja na Kanuni za Kudumu za Baraza hili zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati za Kuchunguza na kudhibiti fedha za Umma kuwa, kazi ya kuzifuatilia ipasavyo ripoti zote sita za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ipo mgongoni mwetu. Ni vyema tukaisaidia nchi yetu kwa maelekezo ya Katiba, Sheria na Kanuni za Baraza la Wawakilishi, juu ya kuzifuatilia na kufanya uchunguzi wa kina kuhusiana na hoja zilizoibuliwa katika ripoti hizo, kwani wananchi wana matumaini makubwa na Kamati zao kuwa zitaibua uhalisia wa yote yaliyotendeka na kila mtu au Taasisi itapata haki

yake kwa mujibu wa kile kilichotendwa.

**Mheshimiwa Spika**, tunaendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Wasaidizi wake kwa kuwa mfano wa kipekee na wa historia wa kuyatafsiri kivitendo maelekezo ya kifungu cha 112(5) juu ya kuwasilishiwa Ripoti hizi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa njia ya uwazi kupitia vyombo tofauti vya Habari. Hali hii imesaidia kukuza utawala bora katika nchi yetu na kuongeza ufahamu wa wananchi juu ya majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar na mambo ambayo baadhi ya watendaji wasiokuwa na nia njema na maendeleo ya nchi yetu wanayoyafanya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inapongeza hatua hiyo na inaomba iendelee kutekelezwa kwa mustakabali mwema wa Zanzibar na Wazanzibari ili hatimae Kamati zetu za Kifedha zenye dhima iliyopewa Kikatiba, Kisheria na Kikanuni kuyathibitisha yale yaliyochunguzwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kuvisaidia vyombo vyetu vya kusimamia Sheria katika kutenda haki kwa waliohusika na kutajwa katika Ripoti hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia naomba kuishukuru Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano mkubwa inayoipatia Kamati yetu wakati wa kutekeleza majukumu yake ukiwemo utekelezaji wa kazi hii ya kuchambua na kutoa maoni ya Kamati juu ya uwasilishaji wa Ripoti hizi za Ukaguzi. Nawashukuru pia Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

……………….
Mhe. Juma Ali Khatib,
Mwenyekiti,
Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC),
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**